TAARIFA YA MAMBO MUHIMU KWA UFUNGUZI WA AKAUNTI

(Itatolewa na kusainiwa kabla ya kufungua akaunti)

Kwa mujibu wa Kanuni ya 27 ya Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania (Kumlinda Mlaji wa Huduma za Fedha), 2019 (Kama zilivyorekebishwa).

Jina la Mtoa Huduma: _____ Jina la Bidhaa: _____ Tarehe ya Kutolewa:_____.

Taarifa Muhimu:

Taarifa hii ya Mambo Muhimu inatoa muhtasari ulio wazi na mfupi wa sifa kuu, faida, ada, tozo, taarifa na athari nyingine zinazohusiana na akaunti hii.

Tafadhali soma taarifa hii kwa makini kabla ya kufungua akaunti. Iwapo, hutaelewa sehemu yoyote, tafadhali muulize mwakilishi wa benki kwa ufafanuzi.

1. Maelezo ya Bidhaa

Akaunti hii imeundwa kuwawezesha wateja kuweka fedha zao kwa usalama, kutoa na kusimamia fedha. Kulingana na aina ya bidhaa, akaunti inaweza kutoa riba, huduma za malipo, na upatikanaji kupitia njia mbalimbali za benki.

2. Mahitaji ya Vigezo Stahiki

Kufungua akaunti hii, lazima uwasilishe vifuatavyo:

(a) Kitambulisho halali

(b) Picha za pasipoti (kama itahitajika)

(c) Fomu ya kufungua akaunti iliyojazwa

(d) Kiasi cha chini cha kufungua (ikiwa kinahitajika)

(e) Uthibitisho wa anwani (ikiwa inahitajika)

3. Sifa Kuu za Akaunti

Kipengele	Maelezo
Aina ya Akaunti	
Sarafu	
Kiwango cha chini cha kufungua	
Kiwango cha chini cha kuendesha akaunti	
Kiwango cha riba (kama kipo)	
Mzunguko wa Malipo ya Riba	
Njia za Upatikanaji wa Huduma	

4. Ada na Tozo (Ikiwemo Kodi Zinazotumika)

Huduma*	**Ada/Tozo**
Ada ya kufungua Akaunti	
Ada ya Usimamizi/kuihudumia Akaunti ya kila mwezi	
Kutoa Fedha kwenye ATM (Benki yako)	
Kutoa Fedha kwenye ATM (Benki nyingine)	
Kutoa Fedha Faunta	

Kuangalia Salio	
Taarifa ya Akaunti	
Utoaji wa Kadi ya ATM	
Kubadilisha Kadi ya ATM	
Uhamishaji wa Fedha kwa Benki kupitia Simu ya Mkononi	
Gharama nyingine (kama zipo)	

5. Vihatarishi na mambo ya muhimu ya Kuzingatia

(a) Ada, tozo na viwango vya riba vinaweza kubadilika kwa taarifa ya awali kulingana na kanuni husika.

(b) Kushindwa kudumisha kiwango cha chini kinachohitajika cha salio kunaweza kusababisha adhabu (ikiwa inatumika).

(c) Akaunti inaweza kuwa isiyotumika (inactive) iwapo hakutakuwa na miamala iliyoanzishwa na mteja kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitano (5) mfululizo, na inaweza kuwa tulivu (dormant) iwapo hakutakuwa na miamala iliyoanzishwa na mteja kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12) mfululizo.

(d) Daima linda namba zako za siri (PIN), nywila na taarifa zako za benki ili kuzuia ufikiaji usioidhinishwa au udanganyifu

(e) Mteja unapaswa kuijulisha taasisi yako kwa maandishi mara moja kuhusu mabadiliko yoyote ya taarifa binafsi (kwa mfano: anwani, namba ya simu, au taarifa za utambulisho)

6. Haki na Wajibu wa Mteja

Haki za mteja:

(a) Kupata taarifa zilizo wazi, sahihi na kwa wakati kuhusu masharti ya akaunti, ada na tozo.
(b) Kupokea taarifa za akaunti na taarifa za miamala.
(c) Haki ya faragha na usiri wa taarifa binafsi na za kifedha.
(d) Kuwasilisha malalamiko na kupokea majibu kwa wakati.

Wajibu wa mteja:

(a) Kutoa taarifa sahihi na kamili wakati wa kufungua akaunti na baada ya hapo.

(b) Kulinda nyenzo zinazotumika kufanya miamala (kadi ya ATM, namba ya siri (PIN), na nywila).

(c) Kukagua taarifa za akaunti mara kwa mara na kutoa taarifa za hitilafu au tofauti zozote kwa wakati.

(d) Kutoa taarifa mara moja endapo kuna shaka ya udanganyifu au miamala isiyoidhinishwa.

7. Kushughulikia Malalamiko

Iwapo una malalamiko yoyote kuhusu bidhaa au huduma hii, tafadhali wasiliana na:

Mtoa Huduma za Kifedha (FSP):

TAARIFA YA MAMBO MUHIMU KWA UFUNGUZI WA AKAUNTI

Kitengo cha Huduma kwa Wateja

Simu: _____ Barua pepe:_____Tawi:_____ .

Mtoa huduma atapokea na kushughulikia malalamiko yako ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Kanuni.

Iwapo hujaridhishwa na utatuzi wa malalamiko yako au haujajibiwa na mtoa huduma ndani ya siku 14, unaweza kuyawasilisha Benki Kuu:

Benki Kuu ya Tanzania:

Kurugenzi ya Ustawi na Huduma Jumuishi za Fedha

Namba ya kupiga Bure: 0800 1111 00

Tovuti: https://semanabot.bot.go.tz

Programu ya simu: *Sema na BoT*

Msaidizi wa mazungumzo kwa njia ya mtandao(Chatbot): **"SEMA"**

USSD**:*152*50#**

8. Tamko la Mteja

Ninathibitisha kwamba:

• Nimepokea, nimesoma na nimeelewa Taarifa hii ya Mambo Muhimu.

• Nimepewa fursa ya kuuliza maswali na nimepata maelezo ya kuridhisha.

• Nakubali kufungwa na masharti na vigezo vya akaunti hii.

Jina:_____ Sahihi: _____Tarehe:_____ .

9. Uthibitisho wa Mtoa Huduma

Tunathibitisha kwamba Taarifa hii ya Mambo Muhimu imetolewa kwa kuzingatia Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania (Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Kifedha), 2019 (kama zilivyorekebishwa)

Jina:_____ Sahihi:_____.

Tarehe: _____ Muhuri:_____ .